


# NGUVU YA KRISMASI KATIKA MAISHA YA MWAMINI : KRISTO KUZALIWA, KUKUA NA KUTAWALA NDANI YETU

## SIKU YA KWANZA

KRISMASI KAMA SIRI YA MBINGUNI ILIYOFICHWA, SASA IKIFUNULIWA

**Lengo la Siku** : Kumsaidia mwamini aelewe kwamba Krismasi ni siri ya Mungu (mystery), si tukio la kawaida. Wakolosai 1:26–27 "siri iliyokuwa imefichwa tangu zamani… Kristo ndani yenu." Rumi 16 :25-26, lakini sasa imefunuliwa ile siri iliyokuwa imefichwa tangu milele, ikadhirishwa kwa. Waefeso 3 :9 siri iliofichwa tangu milele ndani ya mungu.

Siri katika mfumo wa kitheologia inaitwa (MAISTERIO) ni jambo ambalo linafungwa linafichwa linajuwa mwenye nalo mwenyewe. Ao ni jambo ambalo linalofichwa kwa ufahamu, hauwezi kulifahamu.
Siri inaitwa tena (SOD) yaani : ukweli wa mungu uliopo ndani ya baraza ya mungu, unaofichwa humo katika baraza, na hauwezi kufahamu siri hio bila baraza hio kuhusika.
1kor 2 :10 Roho anaweza funulia siri hio kwa wale wamchao peke yake, kwa kuwa roho ni mumoja kati ya ile baraza, ya walinda siri.

UNAITAJI KUFUNULIWA SIRI HIO : Siku zote kama haujue kitu unakuwa mjinga mbele ya kitu hicho. Ukiona mtu ambaye anakuwa na kitu anakuzidia juwa kwamba mtu huyo anayo siri wewe mwenye haufahamu, ndo maana anakuzidi.

MAMBO YA MUNGU NI SIRI : mambo ya mungu ni siri kama mungu hakukufunulia hauwezi kuyafahamu kama yeye hakukufunulia. Na kama utakaa bila kuyafunuliwa utakuwa mkristo ila mjinga katika mambo ya rohoni.
NA WEWE PEKE YAKE UKO SIRI : Wewe mwenyewe ni siri kubwa kama, kama mungu hakufunulie unaweza ukaishi bila kijitambua, ao kujijua wewe mwenye.
Kuna watu wako hapa lakini hawajijue mpaka sasa. Anajiona lakini hajijue. Na kama unaweza kaa bila kujijua hauwezi kufanikiwa katika maisha yako.
Kwa nini ulizaliwa uko mwanamke. Kwa nini uko buterere, kwanini uko mu kanisa hii, karama yako ni gani,.
Kuna vitu vingine unabidi uvifahamu juu yako mwenyewe. Kwanini niko na hii probleme katika maisha yangu. Endapo haujujue mwenyewe, na hauwezi kumfahamu mungu, na hauwezi kuufahamu wokovu, ao ukristo.
FAIDA YA KUJIJUA :

1- Unaweza kujua kusudi la maisha yako
2- Inakusaidia kutovunjika moyo wakati watu wasio kujua wako wanakusema gisi hauko.
3- Kuna mambo mengine hautakuwa unaingia ndani sasabu hayakuhusu.
4- Unaweza ukamjua Mungu na namna ya kutembea na mungu vizuri. Bila kutegemea watu.

KUNA NJIA 3 TATU ZA KUKUWEZESHA KUJUA SIRI USIO IJUA.

1- LEBAB : inatokana na RESISTANCE : kugangania bila kuchoka mpaka ujue siri fulani. Musa alimwambia Mungu siwezi kutembea na mtu ninae msikia ila simuone. Mungu akasema unaomba kitu kigumu ila akazidi kugangania, musa alimuambia mungu ninaitaji kujua jina lako sitaki kwenda na yule nisie jua jina lake.
   Simeoni na annah walibaki kanisani wakisubiri ahadi ya mungu juu yao, wakajua siri wengine walikuwa bado hawajajua.
2- RUAH : Kuchukua hatua juu ya dhambi fulani : kama kuna dhambi ingali inakusumbua hauwezi kujua siri. Sababu zambi huwa inakufupisha, ina kupunguza, inakufifiza, ni ukuta amabo unnaweza tuma usiweze kufunuliwa siri.
   Mfano : yusufu. Alichunga mdomo pamoja na kuararaza maria mungu akamufunulia siri. Hauwezi kufunuliwa siri wakati ungali unaenda unasema wengine mbaya.
3- SYNEIDESIS : siri mtu anaweza kuipata kwa neema : mungu mwenyewe anakufunulia bila hakuna kitu ulifanya. Siri hiyo ni vile tulivyo funuliwa wokovu. Kujua mungu tukakubali kuokoka. Hii ndio siri :
   1kor 1 :18 habari ya msalamba inafichwa kwa wale walio potea ndo maana kwao ni upuuzi lakini kwetu sisi tulio funuliwa ni nguvu za mungu.
   Krismase kwa wamoja ni upagani lakini kwetu kuna siri tulio funuliwa na Mungu.

LEB ESO ANTHROPOS : (kuna mfumo mungu anakuwaga anaongea na watu kupitia moyo wako unasikia moyo wako unakuambia jambo na unalikubali hata kwamba halifafanuke vizuri. 2yoh 2 :20, rom 8 :16

**SIO KILA SIRI YA MUNGU NI LAZMA MWANADAMU AIFAHAMU :**

INAITWA **NISTAROT** : Kumbu 29 :29 mambo ya siri ni ya bwana mungu wetu lakini yale yalio funuliwa ni yetu.

Kama siri hiyo inaweza kukushitua (yesu gestemani)

Kuna mengine mungu anaweza akafanya kwa siri bila kukujulisha unaona yamefanyika hata kwamba mungu hakukuambia, iwe katika ndoto ao kwa namna yoyote.

NISTAROT INAGAWA NDANI VITU 2

1- RAZINI au NISTAROT : mambo ya rohoni ya siri.
2- MASHAL au CHIDOT zab 78 :2 mambo ya siri yanayo funuliwa kwa mifano tu ila hayako wazi.

RAZINI au NISTAROT ni : ufunuo 13 :8, 1petro 1 :19-20

Tangu mwanzo kuwekwa misingi ya ulimwengu : APO KATABOLES KOSMOU : jambo hili lilifanyika tangu kuweka misingi ya ulimwengu. Ao ulikuwa mpango mungu alikuwa nao na ramani yake yose jisi itakavyokuwa. NISTAROT : mambo ya siri ya mungu yenye yeye mwenyewe anajuwa.

**KIPENGELE 1** (UFUNUO ADIMU): KRISMASI SI HADITHI NI MPANGO WA MILELE WA MUNGU

Ufunuo 13:8 “Mwana-Kondoo aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya dunia.”

**Ufunuo:** Yesu alikuwapo kabla ya Bethlehemu tena Krismasi ni mpango wa kabla ya uumbaji.

Mfano : uliumbwa zamamani na kile utakuwa umekifanyika zamani, katika ulimwengu wa roho. Kile ulicho kwasasa ni matokeo ya kile ulicho fanyika zamani. Unaitaji mungu akufunulie siri ya kile uliumbiwa ao kile ulicho fanyika zamani kusudi uanze kukiishi katika maisha yako ao uanze kukifanya.

Kama hautakifanya unafanishwa na kupandwa kwa mbegu ya mzabibu mzuri kunaota mzabibu feki. Ndo maana yesu aliomba sana bwana amutie nguvu ili aweze kutimiza kile alicho fanyika zamani, kitakacho dhihirika katika mwili. Vrs

NINATAKA NIKUTIE MOYO TENA.
➡ Maisha yako hayaanzii kwenye shida ulizonazo
➡ Ulipangwa kabla ya tatizo lako

**KIPENGELE 2** : BETHLEHEMU KAMA MAHALI PA UFUNUO, SI RAMANI : Mika 5:2
Ufunuo: Bethlehemu si eneo tu, ni hali ya moyo. Mungu huchagua vilivyo vidogo ili kuachilia vikubwa.
**Ujumbe wa kinabii:** Mungu atazaa kusudi lake ndani ya udhaifu wako.
KATIKA MFUMO WA KIMUNGU KUNA NAMNA KITU HUANZA KATIKA UDHAIFU HATUA KWA HATUA VINAKUWA NA NGUVU VIKISHA KUKUA.
MFANO MTI MYAMA VIUMBE VYOTE HUANZA KATIKA UDHAIFU KUMALIZA KATIKA NGUVU.
DIVYO MUNGU ANAVYO ENDESHA MAMBO :

**KIPENGELE 3** (KINABII): NYAKATI ZA MUNGU HAZICHELEWI, HUJIFUNUA Luka 2:6
Tangazo la kinabii: Kile kilichoonekana kuchelewa, sasa kimefika wakati wake

**SIKU YA PILI**
**KRISMASI KAMA KUVUNJWA KWA MIFUMO YA GIZA NA MABADILIKO YA UTWALA**
Lengo la Siku : Kumfundisha mwamini kwamba kuzaliwa kwa Yesu kulitikisa falme zisizoonekana. Isaya 9:6

KIPENGELE 1 (ufunuo): **YESU KUZALIWA WAKATI HERODE ANATAWALA** Mat 2:1-3
**Ufunuo:** Krismasi ilikuja wakati wa mfumo wa hofu, mauaji na ukandamizaji. Mungu huzindua wokovu katikati ya giza
**Ujumbe wa kinabii:** Wokovu wako hauzuiliwi na mfumo uliokuzunguka.
KRISMASE NI MWITIKIO WA MUNGU KWA KILIO CHA VIZAZAZI : kutoka 2 :24 mungu akasikia kuugua kwao.
YESU ALIZALIWA KAMA PIA JIBU LA MAOMBI : Luka 2 :25-32 yesu alizaliwa kama jibu la vizazi. Krismase ni ushahidi kwamba mungu hafuti maombi ya kale.
Kuzaliwa kwa yesu ni tumaini jipya ya maombi yalio chelewa kujibiwa.

KIPENGELE 2 (CHA KINA): NYOTA KAMA LUGHA YA MBINGUNI KWA DUNIA Mat 2:2
Ufunuo: Nyota ilikuwa ishara ya wakati (prophetic timing). Mbingu zilikuwa zinatoa taarifa kabla dunia haijajua.

Ujumbe wa kinabii: Mbingu tayari zimeashiria juu ya maisha yako
KIPENGELE 3 : KIFO CHA WATOTO NA VITA YA KIROHO ISIYOONEKANA MAT 2:16
Ufunuo adimu: Kuzaliwa kwa Kristo kulianzisha vita ya kiroho. Giza lilijua tishio kabla nuru haijakua.
Ujumbe wa kinabii: Upinzani uliokutana nao ni uthibitisho wa thamani yako
**SIKU YA TATU**
KRISMASI KAMA MCHAKATO: KRISTO KUZALIWA, KULELEWA NA KUKUA NDANI YA MWAMINI
Lengo la Siku : Kumfundisha mwamini kwamba Krismasi ni mchakato, si tukio la siku moja. Luka 2:40
KIPENGELE 1 (HAKIFUNDISHWI SANA): Yesu Alikua Kimya Kabla ya Kufunuliwa Luka 2:51–52
Ufunuo: Miaka 30 ya ukimya, miaka 3½ ya huduma, Ukuaji hutangulia ufunuo
Ujumbe wa kinabii: Kipindi chako cha ukimya kinakuandaa kwa sauti yako

KIPENGELE 2: YOSEFU KAMA MFANO WA NIDHAMU YA KIROHO Mathayo 1:19–24
Ufunuo: Yosefu aliilinda siri ya Mungu bila kelele. Nidhamu inalinda ufunuo.
Ujumbe wa kinabii: Ukilinda ufunuo, ufunuo utakutukuza

KIPENGELE 3 (KINABII): Kukimbilia Misri: Wokovu kwa Njia Isiyotarajiwa Mathayo 2:13–15
Ufunuo adimu: Misri, mahali pa utumwa, pakawa mahali pa hifadhi. Mungu hubadilisha tafsiri ya mahali.
**Ujumbe wa kinabii:** Mahali palipokuumiza, Mungu anaweza kukuhifadhi.

**SIKU YA NNE**
KRISMASI KAMA MWITO WA KINA: MWAMINI KUWA CHOMBO CHA KUZAA KRISTO KWA ULIMWENGU : **Lengo la Siku** : Kumhamasisha mwamini aishi kama Bethlehemu hai. galatia 4:19

KIPENGELE 1 (UFUNUO WA KINA): Mariamu: Tumbo la Utii, si la Umaarufu Luka 1:38
**Ufunuo:** Mungu anatafuta tumbo la utii, si jukwaa, Utii unazaa Kristo
**Ujumbe wa kinabii:** Utii wako utazaa kile ambacho kizazi chako kinahitaji.
KRISMASE NI KIFO CHA KIBURI NA KUZALIWA KWA UNYENYEKEVU WA ROHO. Filip 2 :7-8
Kuzaliwa kwa yesu ndani ya hori, ni nguvu ya kuuwa roho ya kujikweza kwa mwanadamu. Mungu hushuka pale ego anapo ondolewa mith 16 :18

KIPENGELE 2 (ADIMU): Wachungaji: Ufunuo Huwajia Walinzi Luka 2:8–9
Ufunuo: Wachungaji walikuwa kazini, si madhabahuni, Mungu huwafunulia walinzi, si wavivu.
Ujumbe wa kinabii: Uaminifu wako wa siri unavuta ufunuo wa wazi

KIPENGELE 3 (HITIMISHO CHA KINABII): Kristo Ndani Yako kama Sauti ya Mwisho ya Krismasi, Wakolosai 1:27. **Tangazo la kinabii la mwisho:** Krismasi hii haitakuwa kumbukumbu, itakuwa mabadiliko, Kristo atatawala ndani yako, kupitia wewe, na kwa ajili yako

MWITO WA MWISHO WA KIROHO : Toba ya ndani, Kujitoa upya Maombi ya Kristo kutawala Warumi 8:10.
KIPENGELE CHA 4 : KRISMASE KAMA MLANGO WA MUNGU KUINGIA KATIKA ULIMWENGU WA MWANADAMU : yoh 1 :14 neno akafanyika kuwa mwili, akakaa kwetu
Ufunuo mpya : yesu hakuja duniani kutembea bali kuanzisha makao. Krismase ni malango ya mbinguli kufunguliwa duniani. Mwanzo 28 :17 hapa tunaona mlango wa mbinguni. Mwanadamu ni mahali pa makutano ya mbinguni na duniani. Maombi yake yanapata uzito wa kiroho.